TAFADHALI SOMA MAELEZO KWA MAKINI KABLA YA KUJAZA FOMU

1. **Mtihani wa kujiunga** na shule (Entrance & Interview) **utafanyika SANTHOME SABS Girls' Sec. School, NALA**, DODOMA, Tarehe **10 Decemba 2026, Alhamisi.**
   Mitihani tunaanza saa 2 kamili.
2. **Urudi na fomu ya maombi siku ya mtihani. Fomu ya maombi iambatanishwe na Photo copy ya cheti cha Ubatizo na cheti cha Kuzaliwa.**
3. Fomu isiyo kamili haitapokelewa. **Fomu ziwe original, photo copy haikubaliki. Picha ni lazima**. **Tumia mwandiko unao onekana vizuri kujaza.**
4. Kama ukichelewa kufika kwa wakati siku ya mtihani hutaruhusiwa kufanya mtihani.
5. **Uje na sare ya shule ya msingi uliyosoma siku ya mtihani.**
6. Wanafunzi **waliomaliza darasa la saba tu wanastahili** kuja kufanya mtihani wetu.
7. **Kufaulu mtihani wa Taifa wa darasa la 7 ni muhimu** ili kupata nafasi katika shule ya Sekondari.
8. **Majina ya wanafunzi watakao faulu yatatangazwa tarehe 12 DECEMBA 2026 hapa shuleni saa 3.00 asubuhi, na waliofaulu watajulishwa kwa njia ya SIMU. Pia itapostiwa katika website ya shule.**
9. Kalamu moja inatosha siku ya mtihani.
10. Tutakuwa na **mitihani miwili,** mmoja mchanganyiko na mmoja Hisabati peke yake, pia wote watahojiwa **(personal interview).**
11. Siku ya mtihani, saa sita tutakuwa tumemaliza shughuli zote.
12. Wanafunzi watakaopata **ALAMA za JUU**, ndiyo watakao chaguliwa. Maamuzi ya shule ndiyo ya mwisho katika swala hili.
13. **Mwisho wa kuchukua fomu ni tarehe 09/12/2026 siku ya Jumatano.**
14. **Mtoto mwenye matatizo ya tumbo (Ulcers) au ugonjwa mwingine unao takiwa kuhudumiwa kwa karibu zaidi asije kwenye shule hii ya Bweni. Kwa vile hatutoi chakula cha pekeee. Magonjwa mengine kama asthma, kifafa n. k. hayafai katika Shule ya Bweni.**
15. **Kwa wale wanafunzi ambao wanatoka nje ya Wilaya ya Dodoma ni LAZIMA na vema wawe na mlezi mwenyeji wa hapa Dodoma aliye tayari kufika hapa shuleni wakati wowote anapohitajika**